

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Namba za simu
Mkuu wa Shule 0757783801
Makamu Mkuu wa Shule 0763 896501

Shule ya Sekondari Nsumba,
S.L.P. 4044,
Nyegezi – Mwanza

Tarehe

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
.....
S.L.P.
.....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NSUMBA
HALMASHAURI YA JIJI MWANZA MKOA MWANZA MWAKA 2018**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2017 tahasusi ya Shule ya Sekondari NSUMBA ipo umbali wa Kilometra 10 Kusini mwa mji wa MWANZA. Usafiri wa basi kutoka mjini MWANZA unapatikana katika kituo cha mabasi IGOMBE nauli ni shilingi 400/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe 2/07/2018 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulenii tarehe 02/07/2018. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/07/2018

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare ya shule

- (a) Sare ya shule hii ni Suruali 2 nyeusi (mifuko 3 marinda 2)
- (b) Shati nyeupe 2 mikono mifupi
- (c) Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta (rangi yoyote na fulana (njano)
- (d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
- (e) Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi /khaki za shule
- (f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
- (g) Sweta blue (itakuwa na nembo ya shule)
- (h) Nguo za kushindia T-shirt ya blue (itakuwa na nembo ya shule)
- (i) Tai nyeusi (itakuwa na nembo ya shule)

2.2. Ada na michango ya shule

- (a). Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akauanti ya shule Na. 31101200163 NSUMBA SEKONDARI katika Benki ya NMB (tafadhalii andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

- (i) Shiling 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
- (ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
- (iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
- (iv) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
- (v) Shilingi 2,000/= nembo ya shule
- (vi) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza (Matibabu). (Wanafunzi washauriwe kujinga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya)
- (vii) Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima mock
- (viii) Fedha ya tahadhari 5000/= (haitarejeshwa) Fedha ya michango ilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na.01J1051337700 NSUMBA EK katika benki ya CRDB (Tafadhalii andika jina la kijana kwenye bank pay slip)

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shulenii ni:-

- (i) Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)
- (ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
- (iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
- (iv) Scientific calculator
- (v) Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi $2\frac{1}{2}$
- (vi) Mashuka pair 2 rangi ya kijani, foronya 1, chandarua 1
- (vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
- (viii) Ndoo mbili ndogo zenyne mifuniko
- (ix) Kwanja 1, jembe 1, reki 1 mifagio ya ndani na nje (chelewa yenze mpini).

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- (i) Wizi
- (ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- (iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
- (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- (v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpinga mwalimu au mtu ye yote yule.
- (vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shulenii au kunyoa kwa mtindo uliokubalika na uongozi wa shule.
- (vii) Kufuga ndevu
- (viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- (ix) Uvutaji wa sigara
- (x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja kuoau kuolewa
- (xi) Kushiriki matendo ya uhalisu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi,

- (xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
- (xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- (xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- (xv) Kudharau Bendera ya Taifa
- (xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- (xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**

- (a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- (c) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutembelea mwanafunzi shulenii pamoja na namba zao za simu.

5. Tafadhalii soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule

Jina la Mkuu wa Shule Josephat S Zakeo

Mhuri wa Mkuu wa Shule 
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NSUMBA
S.L.P 4044 NYEGEZI
MWANZA